*Elimu ya Dini ya Kiislamu*

**Madrasa na Shule za Msingi**

# Kitabu cha Kwanza



*Islamic Propagation Centre*

# *Elimu ya Dini ya Kiislamu*

*Madrasa na Shule za Msingi*

## *Kitabu cha – 1*

### *Toleo la pili*

*Islamic Propagation Centre*

*Maarifa ya Uislamu*
*Madrasa na shule za Msingi*
*Kitabu cha kwanza*
*Toleo la pili*

*© Islamic Propagation Centre (IPC)*

*Toleo la kwanza, 2005*
*Nakala 2000*

*Toleo la pili, Januari 2008, Muharram 1429*
*Nakala 1000*

*Kimetayarishwa na kusambazwa na*
*Islamic Propagation Centre,*
*P.O.Box 55105, Simu 022-22450069 Fax 022-2450822,*
*Dar es salaam,*
*Tanzania.*

*Kimechapwa na*
*Afroplus Industries (LTD)*
*P.O. Box 32427, Tel: 022 2773751,*
*Dar es salaam - Tanzania*

## *NENO LA AWALI*

*Shukrani zote anastahiki Allah. Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.*

*Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha kwanza kwa ajili ya watoto wetu wa madrasa na shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.*

*Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa Kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, tawhiid, Fiqhi, Sunnah, Akhlaq na Tarekh.*

*Tunamuomba Allah atujaalie kufikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa Makhalifa wake hapa ulimwenguni.*

*Wabillahit Tawfiiq*

***Mwalimu Mratibu***
*Islamic Propagation Centre*

# *Yaliyomo*

**Neno la Awali** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .(iii)

**SOMO LA KWANZA: QUR'AN** . . . . . . . . . . . . .1

*Herufi za Kiarabu* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .1
*Irabu* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .1
*Matumizi ya Irabu* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .2
*Zoezi la 1.* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .4
*Sak-na* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .6
*Zoezi. la 2* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .6
*Fat-hatain* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .8
*Kas-ratain* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .8
*Dhwammatain* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .9
*Zoezi la 3* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10
*Kuunganisha herufi* . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10
*Jedwali ya Herufi katika nafasi mbali mbali* . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11
*Zoezi la 4* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .14
*Madda* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .14
*Madda ya "Ye Sakna".* . . . . . . . . . . . . . . . . . .15
*Madd ya "Waw Sakna"* . . . . . . . . . . . . . . . . .16

*Zoezi la 5. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18*
*Shadda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19*
*Zoezi la 6 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19*

***SOMO LA PILI: TAWHIID*** *. . . . . . . . . . . . . . . .20*
*Allah ndiye aliyeumba Mbingu . . . . . . . . . .20*
*Allah ndiye muumba wa Ardhi . . . . . . . . . .26*
*Allah ndiye aliyeumba*
*Watu na Wanyama . . . . . . . . . . . . . . . . . . .30*
*Zoezi la 7 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .36*

***SOMO LA TATU: FIQH*** *.................... . . . . . .38*
*Uislamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .38*
*Nguzo za Uislamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .39*
*Shahada . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .39*
*Najisi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .41*
*Kuondoa najisi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .45*
*Adabu za kwenda haja . . . . . . . . . . . . . . . . .46*
*Kutawadha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .49*
*Kutenguka Udhu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .50*
*Zoezi la 8 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .51*

***SOMO LA NNE: AKHALAQ*** . . . . . . . . . . . . . . .*53*
*Usafi* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*53*
*Kupiga Mswaki* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*53*
*Usafi wa mwili* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*55*
*Usafi wa nguo* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*57*
*Faida za usafi* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*59*
*Vyakula Halali na vizuri* . . . . . . . . . . . . . . .*60*
*Adabu za kula* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*62*
*Kula kwa kiasi* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*64*
*Michezo* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*66*
*Zoezi la 9.* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*70*

***SOMO LA TANO: TAREKH*** . . . . . . . . . . . . .*73*
*Mitume wa Allah (s.w)* . . . . . . . . . . . . . . . .*73*
*Tabia ya Mitume* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*73*
*Mitume waliotajwa katika Qur'an* . . . . . .*75*
*Mtume wa kwanza hadi*
*wa mwisho* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*77*
*Zoezi la 10.* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .*81*

# ***Somo la 1 Qur'an***

## ***Herufi za Kiarabu***

*Lugha ya kiarabu imejengwa kwa herufi zifuatazo:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ج | ث | ت | ب | أ | <<< |
| ز | ر | ذ | د | خ | ح |
| ظ | ط | ض | ص | ش | س |
| ل | ك | ق | ف | غ | ع |
| ي | ء | ه | و | ن | م |

## ***Irabu***

*Herufi za Kiarabu husomeka zikiwekwa alama zinazoitwa Irabu. Irabu ni alama zinazowekwa chini au juu ya herufi ili isomeke.*

1. ***Fat-ha*** *[ـَ]ambayo huwekwa juu ya herufi;*
2. ***Kas-ra*** *[ ـِ ]ambayo huwekwa chini ya herufi na;*
3. ***Dhwamma*** *[ـُ]ambayo huwekwa juu ya herufi.*

## *Matumizi ya Irabu*

### *Fat-ha*

*Herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Fat-ha [ـَ] juu yake husomeka kwa sauti ya 'a'*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جَ | ثَ | تَ | بَ | أَ | << |
| زَ | رَ | ذَ | دَ | خَ | حَ |
| ظَ | طَ | ضَ | صَ | شَ | سَ |
| لَ | كَ | قَ | فَ | غَ | عَ |
| يَ | ءَ | هَ | وَ | نَ | مَ |

***Kas-ra***

*Ni herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Kas-ra [ ـِ ] chini yake husomeka kwa sauti ya '**i**'*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جِ | ثِ | تِ | بِ | إِ | << |
| زِ | رِ | ذِ | دِ | خِ | حِ |
| ظِ | طِ | ضِ | صِ | شِ | سِ |
| لِ | كِ | قِ | فِ | غِ | عِ |
| يِ | ءِ | هِ | وِ | نِ | مِ |

## ***Dhwamma***

*Pia herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Dhwamma [ ُ ] juu yake husomeka kwa sauti ya '**u**'*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جُ | ثُ | تُ | بُ | أُ | << |
| زُ | رُ | ذُ | دُ | خُ | حُ |
| ظُ | طُ | ضُ | صُ | شُ | سُ |
| لُ | كُ | قُ | فُ | غُ | عُ |
| يُ | ءُ | هُ | وُ | نُ | مُ |

## ***Zoezi 1:***

*A.Herufi za Kiarabu husomeka zinapowekwa alama zifuatazo:*
*[..........], [..........] na [...........]*

*B.Weka alama ya fat-ha,dhwamma au kas-ra katika herufi za kiarabu ili zisomeke kama ifuatavyo;*

| | | | |
|---|---|---|---|
| **babu** | | **Jibu** | |
| **kisu** | | **siku** | |
| **duka** | | **ghali** | |

*C. Alama zinazowekwa juu au chini ya herufi za kiarabu ili zisomeke zinaitwa ..........................*

*D. Andika maneno yafuatayo kwa herufi za Kiarabu*

| | |
|---|---|
| **kaki** | |
| **mama** | |
| **jawabu** | |
| **adabu** | |
| **kabati** | |

***Sak-na***

*Herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Sak-na [.....ْ.....] juu yake hazisomeki kwa sauti ya dhahiri ila hukatishwa.*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جْ | ثْ | تْ | بْ | أْ | « |
| زْ | رْ | ذْ | دْ | خْ | حْ |
| ظْ | طْ | ضْ | صْ | شْ | سْ |
| لْ | قْ | كْ | فْ | غْ | عْ |
| يْ | ءْ | هْ | وْ | نْ | مْ |

***Zoezi 2:***

*A.Andika maneno yafuatayo yenye herufi za Sak-na kwa herufi za kiarabu:*

| | |
|---|---|
| ***mkuki*** | |
| ***nta*** | |
| ***mkasi*** | |
| ***dhikri*** | |
| ***inzi*** | |

*B.Andika maneno yafuatayo kwa herufi za kawaida*

| | |
|---|---|
| | مْكَلِ |
| | مِلَكَتِ |
| | سَبُنِ |
| | اَتَمْشِكَ |
| | اُنَسِنْزِآ |

## *Fat-hatain*

*Herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Fat-hatain[ ً ] juu yake husomeka kama ifuatavyo:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جً | ثً | تً | بً | أً | << |
| زً | رً | ذً | دً | خً | حً |
| ظً | طً | ضً | صً | شً | سً |
| لً | كً | قً | فً | غً | عً |
| يً | ء | هً | وً | نً | مً |

## *Kas-ratain*

*Herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya* ***Kas-ratain****[ ٍ ] chini yake husomeka kama ifuatavyo:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جٍ | ثٍ | تٍ | بٍ | إٍ | « |
| زٍ | رٍ | ذٍ | دٍ | جٍ | خٍ |
| ظٍ | طٍ | ضٍ | صٍ | شٍ | سٍ |
| لٍ | كٍ | قٍ | فٍ | غٍ | عٍ |
| يٍ | ء | هٍ | وٍ | نٍ | مٍ |

**_Dhwammatain_**

*Herufi za Kiarabu zikiwekwa alama ya Dhwammatain [ٌ........] juu yake husomeka kama ifuatavyo:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| جٌ | ثٌ | تٌ | بٌ | أٌ | « |
| زٌ | رٌ | ذٌ | دٌ | خٌ | حٌ |
| ظٌ | طٌ | ضٌ | صٌ | شٌ | سٌ |
| لٌ | كٌ | قٌ | فٌ | غٌ | عٌ |
| يٌ | ء | هٌ | وٌ | نٌ | مٌ |

**Zoezi 3**:

*Andika maneno yafuatayo kwa kutumia fat-hatain, dhwammatain au kas-ratain, mfano:*

| | | |
|---|---|---|
| | جً ⬅ | جَنْ |
| كُنْ | | رُنْ |
| غَنْ | | بِنْ |
| ثُنْ | | شَنْ |
| سِنْ | | تُنْ |

## ***Kuunganisha herufi***

*Herufi zote za Kiarabu huunganika mwanzo, katikati na mwisho wa neno; isipokuwa herufi zifuatazo:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| و | ز | ر | ذ | د | ا |

*Herufi hizi huunganika na herufi nyingine zikiwa mwisho tu wa neno.*

*Jedwali ya herufi kuonesha zinavyoungana zikiwa katika nafasi mbali mbali katika neno.*

| ***Mwisho*** | ***Katikati*** | ***Mwanzo*** | ***Herufi*** |
|---|---|---|---|
| ـا | - | ا-- | ا |
| ـب | ـبـ | بـ-- | ب |
| ـت | ـتـ | تـ-- | ت |
| ـث | ـثـ | ثـ-- | ث |
| ـج | ـجـ | جـ-- | ج |
| ـح | ـحـ | حـ-- | ح |
| ـخ | ـخـ | خـ-- | خ |

| Mwisho | Katikati | Mwanzo | Herufi |
|---|---|---|---|
| ـد | ـد | د | د |
| ـذ | ـذ | ذ | ذ |
| ـر | ـر | ر | ر |
| ـز | ـز | ز | ز |
| ـس | ـسـ | سـ | س |
| ـش | ـشـ | شـ | ش |
| ـص | ـصـ | صـ | ص |
| ـض | ـضـ | ضـ | ض |
| ـط | ـطـ | طـ | ط |
| ـظ | ـظـ | ظـ | ظ |
| ـعـ | ـعـ | عـ | ع |
| ـغ | ـغـ | غـ | غ |

| *Mwisho* | *Katikati* | *Mwanzo* | *Herufi* |
|---|---|---|---|
| ـف | ـفـ | فـــ | ف |
| ـق | ـقـ | قـــ | ق |
| ـك | ـكـ | كـــ | ك |
| ـل | ـلـ | لـــ | ل |
| ـم | ـمـ | مـــ | م |
| ـن | ـنـ | نـــ | ن |
| ـو | ـو | و | و |
| ـه | ـهـ | هـــ | ه |
| ـي | ـيـ | يـــ | ي |

## *Zoezi 4:*

*A.Unganisha maneno yafuatayo:*

| | | |
|---|---|---|
| شُ غْ لِ | | كَ لَ مُ |
| تَ ث زَ نِ يَ | | رَ خْ بُ |
| جَ وَ بُ | | حَ لِ مَ |
| مْ جِ نِ | | دَ رَ سَ |

## *Madda 1*

*Madda ni alama inayoashiria kurefusha sauti wakati wa kusoma.*

*Madda ya **Alifu** na **Fat-ha** iliyosimama [ٰ...]*
*Alama hii ikiwa mbele ya herufi yenye Fat-ha inaashiria kusoma kwa kuvuta mara mbili, inaitwa “**madda yenye haraka mbili**”*

بَا تَا ثَا جَا حَا خَا دَا ذَا رَا زَا سَا شَا
صَا ضَا طَا ظَا عَا غَا فَا قَا كَا لَا مَا نَا
وَا هَا ءَا يَا

*Pia herufi ya Kiarabu ikiwekwa Fat-ha iliyosimama juu yake inasomwa kwa kuvutwa mara mbili.*

اٰ بٰ تٰ ثٰ جٰ حٰ خٰ دٰ ذٰ رٰ زٰ سٰ
شٰ صٰ ضٰ طٰ ظٰ عٰ غٰ فٰ قٰ كٰ لٰ
مٰ نٰ هٰ وٰ ءٰ يٰ

***Madda ya "Ye Sakna"*** *[ يْ ] na* ***Kas-ra iliyosimama*** *[ ٖ ]*

*"Ye Sekna" ikiwa mbele ya herufi yenye Kas-ra inaifanya herufi hiyo isomwe kwa kuvutwa mara mbili.*

*Mfano:*

بِيْ تِيْ ثِيْ جِيْ

*Pia herufi zikiwekwa Kas-ra iliyosimama juu yake inasomwa kwa kuvutwa mara mbili.*

اٖ بٖ تٖ ثٖ جٖ حٖ خٖ دٖ ذٖ رٖ زٖ سٖ

شٖ صٖ ضٖ طٖ ظٖ عٖ غٖ فٖ قٖ كٖ لٖ

مٖ نٖ هٖ وٖ ءٖ يٖ

***Madda ya Waw Sakna** [ وْ ] ikiwa mbele ya herufi yenye Dwamma inaifanya herufi hiyo isomwe kwa kuvutwa mara mbili.*

*Mfano:*

أُوْ بُوْ تُوْ ثُوْ جُوْ حُوْ خُوْ ...

***Dhwamma iliyosimama*** *[ ٌ ] ikiwa mbele ya herufi yenye Dwamma inaifanya herufi hiyo isomwe kwa kuvutwa mara mbili.*

*Mfano:*

اٌ بٌ تٌ ثٌ جٌ حٌ خٌ دٌ ذٌ رٌ زٌ سٌ

شٌ صٌ ضٌ طٌ ظٌ عٌ غٌ فٌ قٌ كٌ لٌ

مٌ نٌ هٌ وٌ ءٌ يٌ

## *Zoezi 5:*

*A. Soma maneno yafuatayo na kufanya mazoezi ya kuandika hapo chini kwa kuyarudia kama yalivyo:*

| | |
|---|---|
| مٰلِكِ | الْعٰلَمِيْنَ |
| الْكٰفِرُوْنَ | مَالُهٗ |
| الْمَغْضُوْبِ | نَسْتَعِيْنُ |

*B.*______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

## *Madda 2*

*Madda ya kuvuta mara nne [ ٓ ]*
*Alama hii ikiwa juu ya herufi husomwa kwa kuvuta mara nne;Inaitwa "madda yenye haraka nne"*

***Mfano:***

| | | |
|---|---|---|
| لِيَسُوٓءُ | سَآءَ | جَآءَ |
| مَآءَ | سِيٓـَٔتْ | سُحْتٍ |

***Alama ya Shadda*** *[ ـّ ] ikiwekwa juu ya herufi husomwa kwa kukaza:*

*Mfano:*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| اَلَّذِيْنَ | بِشِقِّ | اِنَّهُ | رَبُّكَ | شَقَّ |

## *Zoezi 6:*


*Soma kwa ufasaha maneno yafuatayo:*

| | | |
|---|---|---|
| وَمِنْ شَرِّ | بِرَبِّ | إِيَّاكَ |
| فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّيْنَ | | حَمَّالَةَ |


# Somo la 2 Tawhiid

## Allah ndiye aliyeumba Mbingu

*Nani aliyetengeneza milango na madirisha ya nyumba yenu?*




***Fundi seremala.***



*Nani aliye ujenga msikiti wenu?*

***Fundi mwashi.***

*Na ninani aliyeshona nguo zako?*




***Fundi cherehani.***



*Nani aliyetengeneza viatu vyako?*

***Fundi viatu.***

*Jua halikutengenezwa na mtu bali limeumbwa na Allah.*



*Na Allah ndiye anayelichomozesha jua mashariki na kulizamisha magharibi.*

Waislamu hufuata mwezi katika kuhesabu tarehe.
Mwezi wa Kiislamu una siku 29 au 30.
Mwezi wa Ramadhani ukiandama Waislamu wote huanza kufunga.




Na mwezi wa Shawwal ukiandama wanasherehekea Id-el-Fitri.
Hakuna nguzo inayoshikilia mwezi.
Mwezi huogelea angani bila ya kuanguka.

**Nani aliyeutengeneza mwezi?**

Mwezi haukutengenezwa na mtu bali umeumbwa na Allah.
Na Allah ndiye aliyeupa mwezi uwezo wa kutoa nuru.

*Nani fundi aliyetengeneza nyota zilizopo angani?*
*Allah ndiye aliyeziumba nyota hizo.*
*Vitu tunavyotumia nyumbani vimetengenezwa na mafundi mbalimbali.*



*Madaftari yetu yametengenezwa na fundi wa madaftari.*
*Kalamu tunazoandikia zimetengenezwa na fundi wa kalamu.*
*Kila kitu kilichotengenezwa kina fundi wake aliyekitengeneza.*
*Mafundi wote ni wataalamu. Wanao ujuzi wa kutengeneza vitu.*
***Sasa ni vema tujiulize:***

***Nani fundi wa jua?***
***Nani fundi wa mwezi?***
***Nani fundi wa nyota?***
***Kuna binaadamu mwenye uwezo wa kutengeneza jua na mwezi?***

*Qur'an inatufahamisha kuwa:*
*Jua halikutengenezwa na mtu.*
*Mwezi haukutengenezwa na mtu.*
*Aliyeumba jua ni Allah. Aliyelipa jua mwanga mkali na joto ni Allah.*
*Nazo nyota hazikutengenezwa na mtu. Bali vyote hivi vimeumbwa na Allah.*
*Jua linatoka mashariki kwenda magharibi kwa nguvu za Allah.*
*Aliyeumba mwezi utoao nuru ni Allah.*
*Jua, mwezi na nyota huogelea angani bila ya kuanguka kwa nguvu za Allah.*
*Allahu -Akbar, Allahu–Akbar, Allahu– Akbar.*


*Allah ni mkubwa kweli kweli. Allah ni mwenye nguvu kweli kweli.*
*Allah ni mtaalamu kuliko wataalamu wote.*
*Allah ni Fundi kuliko mafundi wote.*
*Allah ameumba mbingu yenye jua, mwezi na nyota. Kweli Allah ni mwenye uwezo mkubwa na mwenye nguvu kweli.*

تَبَارَكَ ٱلَّذِى جَعَلَ فِى ٱلسَّمَآءِ بُرُوجًا
وَجَعَلَ فِيهَا سِرَٰجًا وَقَمَرًا مُّنِيرًا


*Ni mwenye kutukuka kweli kweli Yule aliyezijaalia nyota mbinguni, na akajaalia humo jua na mwezi unaong'ara.*
*(Qur'an, 25:61)*

# ***Allah ndiye Muumba wa Ardhi***

*Nani aliyetengeza gari hili?*



***Fundi wa magari.***



*Nani aliyeunda Radio hii?*

***Fundi wa radio.***

*Nani aliyeunda ndege hii?*




***Fundi wa ndege.***

***Ni nani aliyeiumba ardhi na kuitandaza?***
*Je, kuna mtu anayeweza kuiumba ardhi na kuitandaza?*

*Ardhini kuna milima mikubwa na midogo. Kilimanjaro ni mlima mrefu kuliko yote Barani Afrika.*



***Ni nani aliyeisimika milima juu ya ardhi?***
***Je, kuna mtu anayeweza kuiumba milima na kuisimika ardhini?***
***Ni nani aliyeumba maji yaliyomo baharini, ziwani na mitoni?***
*Je, kuna mtu anayeweza kuyatengeneza maji na kuyajaza baharini, maziwani, mitoni na mabwawani?*





***Mimea huota ardhini.***

*Je, kuna mtu aliyeotesha miti yote na majani yaliyoko porini?*

*Majibu sahihi ya maswali haya ni kuwa: Hakuna mtu anayeweza kuitengeneza na*

*kuitandaza ardhi.*
*Hakuna mtu aliyetengeneza mlima Kilimanjaro.*
*Hakuna mtu aliyetengeneza maji na kuyajaza baharini, mitoni na maziwani.*

*Hakuna mtu aliyeotesha miti na majani porini.*
***Sasa ni nani basi aliyeumba ardhi, milima, maji na mimea?***

*Qur'an inatufahamisha kuwa:*
*Aliyeumba ardhi na kuitandaza ni Allah.*
*Aliyeiumba milima na kuikalisha juu ya ardhi ni Allah.*

*Aliyetengeneza maji na kuyajaza katika mito, maziwa na bahari ni Allah.*

*Aliyeotesha majani na miti ya aina mbali mbali ni Allah.*

*Allah ametukuka kweli kweli.*
*Allah ni mweza kweli kweli.*
*Allah ni mjuzi kweli kweli.*
*Allah ni mwenye nguvu kuliko wenye nguvu wote.*

الَّذِىْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا........


*(Allah) Ambaye ameziumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake. ...............(Qur'an, 25:59).*

## ***Allah ndiye aliyeumba watu na wanyama***



*Hebu tujaribu kujibu maswali yafuatayo:*
***Kuku ametoka wapi?***
*Kuku ametokana na yai.*
*Yai limetoka wapi?*
*Yai limetagwa na kuku.*
***Yai la kwanza lililotagwa na kuku wa kwanza lilitokea wapi?***
*Lilitokana na kuku wa kwanza.*
*Kuku wa kwanza aliyetaga yai la kwanza alitoka wapi?*
*Alitokana na yai la kwanza.*

*Bila shaka, hapana mwisho wa maswali na majibu haya.*
*Tunaweza kuuliza na kujibu maswali bila kufika mwisho.*
*Labda tujiulize swali la mwisho:*
***Nani aliyemuumba kuku wa kwanza?***



*Ng'ombe ni mnyama anayefugwa.*
*Tunakula nyama ya ng'ombe.*
*Nyama ya ng'ombe ni tamu.*
*Pia tunakunywa maziwa ya ng'ombe.*
*Maziwa ya ng'ombe ni mazuri sana.*

***Ng'ombe ametoka wapi?***
*Ng'ombe amezaliwa na mama yake.*
*Mama yake ng'ombe ametoka wapi?*
*Mama yake amezaliwa na mama yake.*
*Endelea kuuliza na kujibu mpaka uchoke lakini huwezi kupata jibu la mwisho. Tutapata jibu la mwisho iwapo tutauliza swali la mwisho lifuatalo:*
***Nani aliyemuumba ng'ombe wa kwanza?***

*Abdul Azizi ni mtoto wa darasa la kwanza. Anasoma katika Madrasatul-aqswaa. Abdul Azizi siku moja aliulizwa na Ustadhi naye akajibu kama ifuatavyo:*



***Ustadhi: Abdul Azizi umezaliwa na nani?***
***Ustadhi****: Nimezaliwa na mama yangu*
***Abdul Azizi : Mama yako amezaliwa na nani?***
***Ustadhi****: Mama amezaliwa na bibi yangu.*

***Ustadhi: Bibi yako amezaliwa na nani?***
***Abdul Azizi****: Bibi yangu amezaliwa na mama yake.*

***Ustadhi: Mama yake Bibi yako amezaliwa na nani?***
*Maswali haya na majibu yaliendelea mpaka kipindi kikaisha;*

*Labda Ustadh angepata jibu la mwisho kutoka kwa Abdul Aziz kama angemuuliza swali la mwisho lifuatalo:*

*Nani aliyemuumba binadamu wa kwanza?*
*Bila shaka umeshapata majibu ya maswali yaliyoulizwa:*

*1. Nani aliyemuumba kuku wa kwanza?*
*2. Nani aliyemuumba ng'ombe wa kwanza?*
*3. Nani aliyemuumba mtu wa kwanza?*

***Majibu:***
*1. Aliyemuumba kuku wa kwanza ni Allah.*
*2. Aliyemuumba ng'ombe wa kwanza ni Allah.*
*3. Aliyemuumba mtu wa kwanza ni Allah.*
*ALLAH ni Muumbaji mwenye uwezo kweli kweli. ALLAH amewaumba wanaadamu, wanyama, ndege, wadudu na kadhalika.*

*Kweli Allah ni Mwenye kutukuka kweli kweli.*
*Allah ameumba mbingu na ardhi.*
*Allah ameumba watu na wanyama.*
*Allah ameumba kila kitu tunachokiona.*
*Allah ni mjuzi kweli kweli.*
*Qur'an inatufahamisha:*

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُم مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ اسْتَوَىٰ إِلَى
السَّمَاءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ ۚ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٩﴾

*Yeye (Allah) ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, tena akakusudia kuumba mbingu na akazifanya mbingu saba. Naye ndiye ajuaye kila kitu. (Qur'an, 2:29).*

## *Zoezi la 7*

*1. Aliyetengeneza milango na madirisha ya nyumba yenu ni .......*

*.........................................................*

*2. Aliyeshona nguo yako ni ...............*

*.........................................................*

*3. Viatu vimetengenezwa na fundi viatu, lakini jua ......................na Allah (s.w).*

*4. Muumba wa miti na wanyama ni*

*..............................................*

*5. Ni fundi gani aliyetengeneza nyota zilizopo angani?*

*Ni........................................*

*6. Tunakula nyama na tunakunywa maziwa ya ng'ombe. Ni nani aliyemuumba ng'ombe?*

*Aliyemuumba ng'ombe ni ..............*

*7. Binaadamu wa kwanza ameumbwa*

*na.........................................................*

8. *Aliyewaumba watoto wa darasa la kwanza ni ............................*
9. *.................... ni muumba mwenye uwezo kweli kweli.*
10. *Tunafahamishwa katika Qur'an kuwa aliyeiumba ardhi na kutandaza ni ..........................*

# Somo la 3 Fiqh

## *Uislamu*

*Uislamu ni Dini ya Haki.*
*Uislamu ni Dini ya Allah.*
*Uislamu ni Dini iliyofundishwa na Mitume wote.*
*Uislamu ni dini kwa ajili ya Walimwengu wote.*



## ***Nguzo za Uislamu***

*Nguzo za Uislamu ni tano*

1. *Kutoa shahada mbili.*
2. *Kusimamisha Swala tano.*
3. *Kutoa Zakat.*
4. *Kufunga mwezi wa Ramadhani.*
5. *Kuhiji Makka kwa kila mwenye uwezo.*

   *Haya mambo matano huitwa Nguzo za Uislamu.*

## ***Shahada***

*Nguzo ya kwanza ya Uislamu ni kutoa shahada mbili.*

*Shahada ya kwanza ni kusema:*

أَشْهَدُ أَنْ لَّآ إِلَٰهَ إِلَّا اللّٰهُ

*Nashuhudia kuwa Hapana Mungu apasaye kuabudiwa haki ila Allah.*

*Shahada ya pili ni kusema:*

وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللّٰهُ

*Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.*

*Muislamu wa kweli anashuhudia kila akiswali kwa kusema:*



أَشْهَدُ أَنْ لَآ إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ

وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللّٰهُ

*Nashuhudia kuwa Hapana Mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah.*
*Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.*

*Waislamu walioshuhudia kikweli hufuata yale yote aliyowaamrisha Allah na Mtume wake. Pia hujiepusha na makatazo yote aliyoyakataza Allah na Mtume wake.*

## ***Najisi***

*Najisi ni uchafu.*
*Vitu vilivyo najisi ni:*

1. *Haja ndogo ya mtoto, mtu mzima, ng'ombe, mbuzi, kondoo na ya wanyama wengine.*
2. *Haja kubwa ya mtoto, mtu mzima, ng'ombe, kuku, ndege na ya wanyama wengine.*




*3. Damu*

*4.Matapishi*






5. Usaha




6. Kiungo cha mnyama kilichokatwa naye yuko hai



7. Ulevi (pombe za aina zote)






8. Maziwa ya mnyama asiyeliwa (kama maziwa ya punda)



9. Mbwa na kila kinachotokana na yeye.

10. Nguruwe na kila kinachotokana na y eye.




## *Kuondoa najsi*



*Iwapo nguo yako imepakazwa najisi yenye harufu, osha kwa maji safi mpaka iishe harufu. Muislamu akiingiwa na najisi mwilini huisafisha kwa maji safi mpaka harufu na rangi vitoweke.*

## Adabu za kwenda haja:


*Muislamu ni mtu mwenye haya. Haendi haja ovyo-ovyo.. Anaposhikwa na haja ndogo au kubwa hujisaidia mahali pa faragha. Kila nyumba ya muislamu ina choo safi. Muislamu akiingia chooni hutanguliza mguu wa kushoto na kusema.*




بِسْمِ اللهِ "اَللّٰهُمَّ إِنِّيْ أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْخُبُثِ وَالْخَبَائِثِ

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu*
*"Ee Allah, Najilinda kwako na matendo maovu na tabia mbaya" (za kishetani).*

*Muislamu huenda haja ndogo au kubwa kwa kuchuchumaa na kutulizana. Akimaliza haja yake hustanji kwa maji safi.*



*Muislamu akitoka chooni hutanguliza mguu wa kulia na kusema:*

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنِّي الْأَذَى وَعَافَانِي

*"Anayestahiki kusifiwa ni Allah ambaye ameniondolea uchafu na kunipa Afya".*

*Muislamu ni mtu nadhifu.*
*Mara tu anapotoka chooni husafisha mikono yake kwa sabuni.*
*Muislamu akiwa safarini au porini huenda haja mahali pa faragha.*


*Ni vibaya kwenda haja kando kando ya mto au kisima.*
*Vile vile ni vibaya kujisaidia chini ya mti wa kivuli au mti wa matunda.*



*Usijisaidie kwenye mashimo. Humo kuna viumbe wanaoishi na wengine ni wa hatari kama vile nyoka.*
*Ikiwa unajisaidia Porini ambapo hapana maji, stanji kwa karatasi laini mpaka uchafu ondoke. Pia unaweza kutumia mawe au majani makavu mpaka uchafu uishe.*

## *Kutawadha (Kutia Udhu)*

*Kutawadha ni kunawa kwa ajili ya kuswali. Muislamu hutawadha kwa kutia nia au kudhamiria moyoni kuwa anatawadha kisha hufanya yafuatayo:*



*Kusema,Bismillahi kuosha viganja vya mikiono mara tatu*



*Kusukutua maji mdomoni mara tatu*




*kuvuta maji puani*



*Kuosha uso maratatu*



*Kuosha mkono wa kulia mpaka kwenye fundo mbili maratatu*



*Kuosha mkono wa kushoto mpaka kwenye fundo mbili maratatu*



Kupaka maji kichwani



Kuosha masikio mara tatu



Kuosha mguu wa kulia halafu wa kushoto mpaka kwenye fundo mara tatu

## ***Kutenguka Udhu:***

*Udhu hutenguka kwa:*

1. *Kwenda haja ndogo au kubwa*
2. *Kutokwa na upepo nyuma.*
3. *Kushika utupu wa mbele au wa nyuma kwa kiganja cha mkono.*
4. *Kulala usingizi.*

## Zoezi 8

1. Dini ya Haki ni dini ya……………………..............
2. Nguzo ya kwanza ya Uislamu  ni …….................

   ..........................................................................

   na nguzo ya tano ni …………………….............
3. Mitume wote wamefundisha dini ya ...............

   ……………………………...............................
4.  Kutoa shahada ni kusema……………...............
5. Aliyeshuhudia kwa kweli hufuata.....................
   na hujiepusha na ....…….......................................
6. Katika Uislamu  najisi ni ……………….........
7. Taja vitu vitano vilivyo najisi:
   - (i) ………………………….
   - (ii) ……………………….…
   - (iii) ……………………….…
   - (iv).……………………….…
   - (v).……………………….…
8. Najisi huondolewa kwa kutumia ……..............

   ..........................................................................
9. Muislamu akiingia chooni hutanguliza

*mguu wa ………………….. na kutoka chooni kwa kutanguliza mguu wa*

*…………………………..........................................*

*10. Muislamu ni mtu ……………………….*

*hivyo haendi haja hovyo.*

*11. Muislamu hutia udhu kwa:*

*(i)kutia nia moyoni.*

*(ii)………………………………......*

*(iii)……………………………….*

*(iv)Kuosha uso mara tatu.*

*(v)……………………………….*

*(vi)………………………………..*

*(vii)Kuosha masikio mara tatu.*

*(viii)……………………………….*

*12. Andika vitu 4 vinavyotengua udhu:*

*(i) …………………………………….*

*(ii)……………………………………..*

*(iii)……………………………………..*

*(iv) ……………………………………..*

# Somo la 4 Akhlaq

## *Usafi*

*Uislamu ni Dini ya usafi.*
*Kila Muislamu yampasa awe safi.*
*Uislamu wa mtu haukamiliki mpaka awe msafi wa mwili, nguo na mazingira yake.*

### ***Kupiga mswaki.***



*Ali ni mtoto msafi.*
*Hupiga mswaki kila asubuhi mara tu anapoamka.*
*Ali ana kawaida ya kulala mchana baada ya kuswali adhuhuri*
*Akiamka usingizini hupiga mswaki kabla hajafanya lolote.*



*Ali hupiga mswaki kila baada ya kula.*
*Pia Ali hupiga mswaki kila mara kabla ya kuanza kutawadha.*
*Hivi ndivyo alivyokuwa akifanyaMtume Muhammad (s.a.w).*
*Muislamu daima humuiga Mtume (s.a.w).*

*Kupiga mswaki husafisha meno.*
*Meno ya Ali ni meupe na safi.*
*Mdomo wa Ali haunuki kwa sababu hupiga mswaki mara kwa mara.*
*Ali anapendwa na Allah.*

*Allah huwapenda watu wasafi wajitakasao.*
*Watoto wasiopiga mswaki huoza meno.*

*Midomo yao hutoa harufu mbaya: Hakika watoto wachafu hawapigi mswaki, hawapendezi na hawapendwi.*

***Usafi wa mwili.***



*Ali kila anapoamka asubuhi hupiga mswaki. Kisha hukoga vizuri kwa sabuni. Ali hukoga kila anapotoka shuleni. Kila baada ya kazi au mchezo Ali hukoga. Pia Ali hukoga kabla ya kulala usiku. Baada ya kukoga Ali huchana nywele zake vizuri.*

*Sauda ni dada yake Ali. Naye ni mtoto msafi kama Ali.*

*Hupiga mswaki na kukoga vizuri mara kwa mara.*
*Hukata kucha zake kila zikiwa ndefu akianza na mkono wa kushoto kidole cha shahada hadi kidole kidogo, kisha mkono wa kulia kidole kidogo hadi kidole gumba na kumalizia kidole gumba mkono wa kushoto.*
*Husuka vizuri nywele zake.*
*Kweli Ali na Sauda ni watoto wazuri na wasafi.*
*Allah huwapenda watoto wazuri wajitakasao.*

*Kila siku ya Alkhamisi asubuhi Ali hukata kucha zake za mikononi na miguuni, kwani ndivyo Mtume (s.a.w) alivyotufunza.*
*Ali akienda haja huwa mwangalifu ili asijipakaze najisi.*



*Hujitwaharisha vizuri kwa maji. Najisi ni uchafu mbaya sana. Mtu mwenye najisi mwilini au nguoni haruhusiwi kuswali.*

*Watoto wachafu wasiopiga mswaki, wasiokoga mara kwa mara, wasiochana nywele zao na wasiokata kucha zao hawapendwi na waalimu wao. Hawapendwi na watoto wenzao. Pia Allah hawapendi watu wasiojisafisha na kujitakasa.*

## *Usafi wa nguo*

*Ali ni mtoto wa darasa la kwanza hajaweza kufua vizuri lakini ni msafi sana. Hachafui ovyo nguo zake. Mama yake humfulia vizuri nguo zake na kuzipiga pasi. Ali akivalia nguo zake hupendeza sana.*

*Ali akienda haja huwa mwangalifu sana, ili asipakaze nguo zake najisi.*
*Nguo yenye najisi ni nguo chafu hata ikiwa inag'ara. Nguo yenye najisi haifai kuswalia.*




*Sauda ni mtoto wa darasa la tatu. Ni mtoto hodari sana anaweza kufua nguo zake vizuri na kuzipiga pasi. Sauda kila mara huvalia nguo safi na kupendeza kila mara huwa*



*mwangalifu nguo zake zisifikiwe na najisi. Allah anawataka Waislamu wavalie nguo safi na nzuri. Anawataka wavalie nguo nzuri zaidi*

*Allah anatuhimiza katika Qur'an:*

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمۡ عِندَ كُلِّ مَسۡجِدٖ ..........

*Enyi wanadamu; Chukueni mapambo yenu katika kila sala…............." (7:31)*



## ***Faida za usafi.***

*Mtoto msafi hupendeza*
*Mtoto msafi hupendwa na watu*
*Mtoto msafi huwa na afya njema*
*Mtoto msafi huwa ni mwenye furaha*
*Mtoto msafi hupendwa na Allah*

## *Vyakula Halali na Vizuri*


*Uislamu ni dini nzuri inahimiza kula vyakula vizuri vilivyo vya halali.*

*Vyakula vizuri ni vile vinavyotuletea afya nzuri.*




*Vyakula vyote visivyo haramu ni vyakula halali.*

*Nyama ya nguruwe ni chakula haramu.*





*Nyama ya mzoga ni haramu.*
*Mzoga ni mnyama aliyekufa bila ya kuchinjwa.*
*Mbuzi, kondoo au kuku aliyekanyagwa na gari akafa bila kuchinjwa ni mzoga.*



*Kuku, mbuzi, au ng'ombe aliyechinjwa na asiye muislamu nyama yake ni haramu.*
*Chakula cha wizi ni haramu.*

*Damu ni kinywaji haramu.*
*Pombe ni kinywaji haramu*
*Aina zote za pombe; bia, mvinyo, kangara, mbege, ulazi ni haramu.*



## ***Adabu za kula***

*Yusuf ni mtoto mzuri na mtulivu. Anaposikia njaa hapigi kelele. Hutulia mpaka chakula kiwe tayari.*

*Yusuf ni mtoto mwenye busara.*

*Yusuf anakula Kiislamu*

*Hunawa mikono yake vizuri kabla ya kuanza kula.*

*Hunawa kwenye maji yanayotiririka*

*Yusuf huanza kula kwa jina la Allah*

*Anapoanza kula husema:*



بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

***Bismillahir-Rahmaanir Rahiim***

***Naanza kula kwa jina la Allah mwingi wa Rehema, mwenye kurehemu.***

*Tunaposahau kusema Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim wakati wa kuwanza kula, tukikumbuka tuseme:*

| بِسْمِ اللَّهِ فِي أَوَّلِهِ وَآخِرِهِ. |
|---|

***Bismillahi Fii Awalihi wa aakhirihi***

***Naanza kula kwa jina la Allah mwanzo wake na mwisho wake.***

*Mtume (s.a.w) ametufundisha kusema hivyo.*

*Yusuf hula kwa utulivu.*
*Humega matonge kwa kadiri.*
*Humega sehemu iliyo mbele yake.*
*Hula na kunywa kwa mkono wa wa kulia*

*Mtume (s.a.w) amekataza kumega matonge hapa na pale.*
*Pia ametukataza kumega matonge makubwa kupita kiasi.*



***Kula kwa kiasi***

*Yusuf hula kwa kiasi, hali akashiba sana.*
*Kushiba sana hukosesha raha.*
*Mtoto anayeshiba sana huwa mvivu.*
*Huumwa na tumbo mara kwa mara.*
*Mtoto wa Kiislamu hashibi kupita kiasi.*
*Allah hawapendi watu walao kupita kiasi.*

*Baada ya kula ni vyema kunywa maji. Yusuf hunywa maji kidogo kidogo. Hanywi yote kwa pupa mara moja. Yusuf humuiga Mtume Muhammad (s.a.w) alivyokuwa akinywa. Hunywa kwa mkono wa kulia Yusuf akimaliza kula au kunywa humshukuru Allah kwa kusema:*

| |
|---|
| اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ اَطْعَمَنَا وَسَقَنَا وَجَعَلَنَا مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ |

*Shukurani njema anastahiki Allah Bwana na (Mlezi wa walimwengu wote). Ambaye ametulisha na akatunywesha na akatujalia kuwa miongoni mwa waislamu*

*Baada ya kumshukuru Allah, Yusuf pia humshukuru mama aliyemwandalia chakula. Humwombea dua, husema:*

جَزَاكِ اللَّهُ خَيْراً.


*Jazaaki Allah Khairan*
*Allah akulipe kwa huduma yako njema.*

*Baada ya kula Yusuf hunawa mikono yake vizuri.*
*Huondoa vyombo na husafisha meza au jamvi vizuri.*

***Michezo***
*Michezo ni muhimu kwa watoto.*
*Huwafanya wawe wachangamfu.*
*Huwafanya wawe hodari.*

*Pia michezo huwafanya watoto wawe wakakamavu.*
*Michezo inaleta upendo na uhusiano mwema.*

*Uislamu unawataka watu wachangamfu, wakakamavu na hodari.*
*Uislamu pia unatuhimiza tupendane na kushirikiana katika mambo mema.*




*Michezo mizuri kwa watoto wa Kiislamu ni mazoezi ya viungo, michezo ya mieleka.*
*Michezo ya mbio*
*Michezo ya kulenga shabaha.*
*Michezo ya kutupa mikuki.*

*Michezo mbali mbali inayochezwa pamoja kama kubebana, kuvutana kwa kamba na mengineyo.*

*Uislamu unaruhusu michezo yote*

*inayowafanya watoto wote wawe wachangamfu, wawe hodari, wawe wepesi na shupavu, wapendane na washirikiane.*



*Watoto wazuri wa Kiislamu hawachezi nyumbani kwa watu wala hawachezi barabarani, wala katika sehemu zilizo katazwa. Watoto wa Kiislamu hawachezi darasani au msikitini, bali hucheza kwenye viwanja maalum vya kuchezea watoto vilivyo karibu na nyumbani au shuleni.*

*Mtoto wa Kiislamu hucheza na watoto wenye tabia nzuri.*
*Hucheza na watoto wenye huruma, heshima,*

*utii, ushirikiano na upendo.*
*Mtoto wa Kiislamu hujiepusha kucheza na watoto wabaya.*
*Watoto wabaya ni wale wenye tabia ya kikatili, sugu, wasiokanyika, wezi, wavuta bangi na wenye matusi.*

*Watoto wabaya ni hatari. Huwapoteza watoto wazuri. Uislamu hauruhusu watoto kucheza michezo mibaya inayopoteza muda kama vile mchezo wa karata, dama, bao na gololi. Pia michezo mibaya ni ile inayosababisha ugomvi na uhasama kama vile michezo ya pata-potea, michezo ya kutaniana, michezo ya mashindano na mengineyo.*
*Watoto wazuri wa Kiislamu hawaendi kucheza mpaka wapewe ruhusa nyumbani.*

## *Zoezi 9*

*1. Uislamu hukamilika kwa mtu kuwa msafi wa ………………………………………………………… na mazingira yake.*

*2. Tunasafisha meno kwa kutumia ……………….… na ……………………..*

*3. ………………………… ni dini ya usafi.*

*4. Mtoto asiyepiga mswaki meno yake ………………………………………………………………*

*5. Ali na Sauda wanapoamka asubuhi huwa wanafanya nini?*

*(i) ……………………………………………..*

*(ii) ……………………………………………..*

*(iii) …………………………………………….*

*6. Kucha ndefu huhifadhi ………………………….*

*7. Muislamu mwenye uchafu mwilini au nguoni haruhusiwi ……………………………………*

*8. Faida za usafi ni……………………………………… ………………….kuwa mwenye furaha na ……………………..na Allah (s.w).*

*9. Uislamu unatuhimiza kula vyakula ……………......na ……………………………………*

*10. Vyakula hivi ni haramu:*

*(i)Nyama ya mzoga*

…………………………………………......

…………………………………………......

…………………………………………......

..........................................................................

*11. Muislamu anapoanza kula husema ................ ……………………………………...........................................*

*12. Mtume Muhammad ametukataza kumega matonge makubwa. Pia amekataza kula ..................................*

*13. Fatuma ni mtoto mzuri, akimaliza kula husema………………………….......................... kisha humshukuru mama yake kwa kusema ……………………………..........*

*14. Mchezo ni muhimu kwa watoto kwani huwafanya wawe ……………………….... pia wawe na mahusiano mema na*

*upendo kwa watoto wenzao.*

15. *Taja michezo inayofaa kwa watoto wa Kiislamu*
    - *(i)* ……………………………………………
    - *(ii)* ……………………………………………
    - *(iii)*……………………………………………
    - *(iv)* ……………………………………...........
    - *(v)* ……………………………………...........

16. *Taja michezo isiyofaa kwa watoto wa kiislamu*
    - *(i)* ..........................................................................
    - *(ii)* ........................................................................
    - *(iii)* .......................................................................
    - *(iv)* .......................................................................
    - *(v)* ........................................................................

# Somo la 5 Tarekh

## *Mitume wa Allah (s.w)*

*Mitume wa Allah (s.w) ni binaadamu kama sisi. Ni binaadamu wanaume walioletwa na Allah (s.w) kuwafundisha watu Uislamu.*

*Uislamu unawafanya watu waishi kwa furaha na amani ya kweli.*

*Furaha na amani ya kweli haipatikani mpaka watu wamtii na kumnyenyekea Allah (s.w). Kumtii na kumnyenyekea Allah (s.w) ni kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote.*

### *Tabia ya Mitume*

*Mitume wa Allah (s.w) walikuwa watu wazuri sana. Tabia nzuri ya Mitume iliwavutia watu wote katika jamii. Mitume wa Allah waliwafundisha watu kuishi vizuri Kiislamu.*

*Mitume wote walikuwa ni wa kweli, waaminifu, waadilifu, wenye huruma, wakarimu, wapole, wavumilivu, wacheshi, hodari, shujaa, na tabia nyingine zote zilizo nzuri.*

*Mitume wote waliepukana kabisa na tabia mbaya kama vile kusema uwongo, kusengenya, kudhulumu, kupendelea na tabia nyingine zilizo mbaya kama hizi. Mitume wenyewe wamekuwa ni mifano bora ya kuigwa katika kuishi vizuri. Kuhusu tabia ya Mtume Muhammad (s.a.w) tunafahamishwa katika Qur'an:*

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ

*Na bila shaka (Ewe Muhammad) unatabia njema kabisa. (68:4)*

## ***Mitume Waliotajwa katika Qur'an.***

*Allah (s.w) anatupenda sana.*
*Ametuletea mitume wa kutuongoza ili tuishi kwa furaha na amani. Mitume wameletwa kwa watu wote.*
*Tunafahamishwa katika Qur'an:*

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا

*"Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila Umma….(16:36).*

*Mitume waliotumwa kwa watu wa mwanzo hadi hivi leo ni wengi sana. Idadi yao anaijua Allah (s.w) pekee.*
*Ni Mitume 25 tu waliotajwa katika Qur'an. Majina yao ni:*

*1. Adam (a.s)*
*2. Idrisa (a.s)*
*3. Nuhu (a.s)*
*4. Hud (a.s)*
*5. Saleh (a.s)*
*6. Ibrahim (a.s)*
*7. Lut (a.s)*
*8. Ismail (a.s)*
*9. Dhulkifly (a.s)*
*10. Dawud (a.s)*
*11. Is'haq (a.s)*
*12. Yaqub (a.s)*
*13. Ayyub (a.s)*
*14. Shuayb (a.s)*
*15. Musa (a.s)*
*16. Harun (a.s)*
*17. Yusuf (a.s)*
*18. Al-yasaa (a.s)*
*19. Sulaiman (a.s)*
*20. Il-yasa (a.s)*
*21. Yunus (a.s)*
*22. Zakaria (a.s)*
*23. Yahya (a.s)*
*24. Isa (a.s)*
*25 Muhammad (s.a.w)*

*Mitume wote hawa walikuwa Waislamu waliofundisha Uislamu na waliishi Kiislamu. Hakuna Mtume wa Allah (s.w) aliyefundisha watu dini ya Ukristo.*

*Allah (s.w) hakuwatuma Mitume kufundisha*

*watu dini isiyokuwa ya Kiislamu. Tunajifunza katika Qur'an kuwa:*

| إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ |
| --- |

*Hakika dini mbele ya Allah ni Uislamu (3:19).*

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي
ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ

*Na anayetaka dini isiyokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake (Allah). Naye Akhera atakuwa na hasara kubwa (3:85)*

## ***Mtume wa Kwanza Hadi wa Mwisho***

*Adamu (a.s) ndiye aliekuwa mtu wa kwanza. Yeye pamoja na Hawwa, mkewe, waliumbwa na Allah (s.w) wakiwa watu kamili.*

*Watu hawa wa mwanzo ambao ni Adam na Hawwa, hawakutokea kwa bahati nasibu. Adam na Hawwa hawakutokana na nyani, bali waliumbwa na Allah (s.w).*
*Hawa ndio watu wa kwanza kuja hapa duniani. Allah (s.w) hakuwaleta Adam na Hawwa duniani kwa lengo la kuwaadhibu. Aliwaleta duniani ili wawe Makhalifa wake.*

*Allah (s.w) aliwaeleza Malaika lengo hili kabla ya kumuumba Adam (a.s). Allah (s.w) akawaambia Malaika kuwa:*

إِنِّي جَاعِلٌ فِي ٱلْأَرْضِ خَلِيفَةً

*Hakika Mimi ni mwenye kumuweka Khalifa katika dunia (2:30)*

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلْأَسْمَآءَ كُلَّهَا

*Na (Allah) akamfundisha Adam majina ya vitu vyote (2:31)*

*Kwa hiyo, mtu wa kwanza, ambaye ni Adam alikuwa na ujuzi wa vitu vyote vya duniani. Aliyafahamu mazingira yake na kanuni zote za maumbile vizuri.*

*Elimu hii ilimfanya Adam (a.s) kuwa kiongozi bora wa familia yake. Hivyo, Allah (s.w) alimteuwa Adam (a.s) kuwa Mtume wake wa kwanza.*

*Mtume Adam (a.s) alikuwa ndiye Muislamu wa kwanza. Yeye pamoja na familia yake waliishi Kiislamu kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w).*

*Lakini baada ya kufariki Mtume Adam (a.s), walitokea watu wabaya katika kizazi chake. Watu hawa walipotosha mafundisho sahihi ya Uislamu. Mafundisho sahihi ya Mtume Adam (a.s) yalipofifia au kupotea kabisa, Allah (s.w) alimleta Mtume mwingine.*

*Mtume huyo alifundisha Uislamu. Na baada ya Mtume huyo kufariki dunia, na kupita muda mrefu, walitokea tena wakorofi kuvuruga dini ya Allah (s.w).*
*Vivyo vivyo, Allah (s.w) alileta Mtume mmoja baada ya mwingine ili kufundisha Uislamu upya baada ya kupotoshwa.*

*Mtume wa mwisho ni Muhammad (s.a.w). Yeye amekuwa Mtume wa watu wote. Ni Mtume wa dunia nzima. Allah (s.w) hata tuma Mtume mwingine baada ya Muhammad (s.a.w). Muhammad (s.a.w) ni Mtume wa mwisho, na hakuna Mtume mwingine baada yake.*

*Habari za Muhammad (s.a.w) tutazipata kwa urefu katika kitabu cha pili.*

***Zoezi la 10***

*1. Mitume wa Allah (s.w) ni wanaadamu wanaume walioletwa kuwafundisha watu……………………………………………*

*2. Kumtii na kumnyenyekea Allah (s.w) ni ………………………………………………….. na ………………. kuacha makatazo yake.*

*3. Tunajifunza vipengele vya tabia nzuri kutoka kwa Mtume wa Allah (s.w). Taja vipengele vitano tu vya tabia njema.*

*(i) ………………………………………………..*

*(ii)……………………………………………..*

*(iii) ……………………………………………..*

*(iv)……………………………………………..*

*(v) ……………………………………………..*

*Wabillah Tawfiiq*